

## MKATABA WA KUPANGISHA YARD

Mkataba huu umetayarishwa hapa Mwanza leo tarehe **17 mwezi 8 mwaka 2018**

### **BAINA YA**

**ABUBAKARI YUSUFU ABUU** wa **S.L.P 1501 MWANZA** (Ambaye katika mkataba huu ataitwa "**MPANGISHAJI**") kwa upande mmoja.

### **NA**

**HUANG XIUYONG** wa **S.L.P 369, MWANZA** ambaye katika makataba huu ataitwa "**MPANGAJI**") kwa upande mwingine.

**NAKUWA;** mwenye nyumba na mpangishaji ni mmiliki halali wa **YARD ILEMELA PLOT No 30 BLOCK 'E.'**

**NAKUWA;** Mpangishaji anataka kumpangisha **YARD** mpangaji amekubali kupanga kwa masharti yafuatayo;-

### **HIVYO PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

1. Kodi ya upangaji wa **YARD** ni kiasi cha **(Tsh5,000,000/=)** **Shilingi Milioni tano tu** kwa mwaka
2. Kipindi cha upangaji kitakuwa ni miaka **mitano (5)** kuanzia tarehe **01/10/2018** hadi tarehe **30/09/2023**.
3. Mpangaji atalipa kodi ya mwaka mmoja ambayo ni milioni tano tu (**tsh 5,000,000/=**) ya kuanzia tarehe **01/10/2018** hadi tarehe **30/09/2019**.
4. Mpangaji atalipa kodi ya mwaka wa pili na wa tatu kwa pamoja yaani shilingi milioni kumi (**tsh 10,000,000/=**) ya kuanzia tarehe **01/10/2019** hadi tarehe **30/09/2021**. Kodi hii italipwa kabla ya mwaka wa pili wa upangaji kuanza.
5. Mpangaji atahusika kulipa gharama za umeme na maji atakayo tumia kipindi chote cha upangaji.
6. Mpangaji anatakiwa kuhakikisha anaweka eneo lake katika hali ya usafi kimazingira.
7. Mkataba unaweza kuongezwa upya mara kipindi cha upangaji kitakapo kwisha kwa maelewano mapya.
8. Taarifa ya miezi mitatu (3) itatolewa kabla ya kuisha kwa mkataba huu na upande mmoja kwenda upande mwingine kuhusu kuendelea au kutoendelea na mkataba wa upangaji.
9. Mpangaji anatakiwa kutunza vizuri **YARD** na mazingira yanayotuzunguka, na atakapoondoka aache **YARD** katika mazingira mazuri na masafi.

**MWANZA**  
28/8/2018

10. Mkataba unaweza kusitishwa iwapo mpangaji hatozingatia makubaliano ya mkataba.
11. Mpangishaji atajenga uzio na kufanya wiring kwa ajili ya kuweka taa juu ya ukuta na nyaya za chuma kwa ajili ya usalama.
12. Mpangishaji atasafisha eneo na kuweka yard katika level moja
13. Mpangishaji atafanya matengenezo katika nyumba ya kuishi.
14. Mpangishaji atafungua maji ya mwauwasa
15. Mpangishaji atajenga godown lenye ukubwa wa 600sqm,
16. Mpangishaji na mpangaji watachangia gharama za kubadilisha matumizi ya kiwanja kutoka residential kwenda light industrial
17. Mpangaji atavuta umeme mkubwa na kuweka transformer kwa gharama zake.
18. Mpangaji atakapoondoka kama ataacha transformer basi mpangishaji atamlipa nusu ya gharama ya transformer ambayo ni kiasi cha milioni 9 za kitanzania (tsh 9,000,000/=)

Utunzaji wa **YARD** ndani na nje ni jukumu la mpangaji mwenyewe, mpangaji anatakiwa kulipa bili ya maji na umeme pindi awamo ndani ya **YARD**, na ahakikishe analipa madeni yote pindi amalizapo mkataba.

**KWA KUTHIBITISHA** yote haya yaliyo tangulia pande zote husika zinaweka saini zao katika mkataba huu kama inavyoonekana.

JINA LA MPANGISHAJI.....*Abubakar Yusuf*.....SAHIHI.....*[Signature]*

1. SHAHIDI WA MPANGISHAJI.....*SUBEI TWAHA*.....SAHIHI.....*[Signature]*

2. SHAHIDI WA MPANGISHAJI.....*OMAR AWAHA*.....SAHIHI.....*[Signature]*

JINA LA MPANGAJI.....*Xiu Yong Huang*.....SAHIHI.....*[Signature]*

1. JINA LA SHAHIDI WA MPANGAJI.....*PETER S. LAIZER*.....SAHIHI.....*[Signature]*

2. JINA LA SHAHIDI WA MPANGAJI.....*ROSE SHELWETE*.....SAHIHI.....*[Signature]*

MBELE YANZI:-  
 JINA:- *BAHATI CHIROPO*  
 ANWANI:- *SUP 13 MUSAHA*  
 CHEO:- *RESIDENT*  
 SAINI:- *[Signature]*  
 TARHE:- *28/08/2018*

